

# Je, Wajua Mtoto Wako Anaweza Kupata Chanjo Bila Malipo?

## Chanjo za Watoto Zinaweza Kusaidia

**Mpango wa Chanjo kwa Watoto (VFC) hutoa chanjo bila malipo kwa watoto wanaostahiki. Takriban nusu ya watoto walio na umri wa chini ya miaka 19 hupokea chanjo ya VFC.**

### Je, mtoto wangu anastahiki mpango wa VFC?

Watoto wanastahiki ikiwa hawajafikisha miaka 19 na:

- Wanastahiki kupokea Medicaid,
- Hawana bima, au
- Ni wa asili ya Wahindi Wamarekani au wa Asili ya Alaska

Watoto ambao bima yao hailipii baadhi ya chanjo au chanjo zote zinazopendekezwa kila mara (wasio na bima kamili) bado wanaweza kupata chanjo kuititia VFC iwapo wataenda katika Kituo cha Afya Kilichoidhinishwa na Serikali ya Kitaifa au Kliniki ya Afya Vijijini.

### Ninaweza kumpeleka wapi mtoto wangu apate chanjo?

- Uliza kama daktari au muuguzi wa mtoto wako ni mto huduma wa VFC. Kitaifa, maelfu ya watoa huduma za afya wamesajiliwa katika mpango wa VFC.
- Ikiwa mtoto wako hana daktari, uliza kama idara ya afya ya umma ya eneo lako inatoa chanjo.
- Tembelea Kituo cha Afya Kilichoidhinishwa na Serikali ya Kitaifa (FQHC) au Kliniki ya Afya ya Vijijini (RHC).

### Nitahitajika kulipa kiasi gani?

- Chanjo zote zinazopendekezwa zinatolewa na Mpango wa VFC bila malipo.
- Madaktari wanaweza kutoza ada kutoa kila chanjo. Hata hivyo, hawaweza kukataa kumchanja mtoto wako ikiwa huwezi kulipia ada hizi.
- Daktari anaweza kutoza ada za ziada kwa ziara ya ofisini au kwa huduma zisizo za chanjo kama vile kipimo cha macho au cha damu.

### Ninaweza kupata wapi taarifa zaidi?

- Uliza daktari wa mtoto wako kama anashiriki katika mpango wa VFC.
- Ikiwa huna daktari wa kawaida:
  - Nenda kwenye kiungo kilicho hapa chini ili uone watoa huduma wanaopatikana katika eneo lako au uchangانue msimbo wa QR ulio upande wa chini kushoto:  
<https://www.health.pa.gov/topics/programs/immunizations/Pages/VFC.aspx>
  - Piga simu 1-877-PA-HEALTH upate mto huduma aliye karibu nawe ambaye amesajiliwa katika VFC.  
\*\*Wakazi wa Philadelphia - piga simu 215-685-6498 upate mto huduma aliye karibu nawe ambaye amesajiliwa katika VFC.
  - Wasiliana na [idara ya afya ya eneo lako](#).
  - Tembelea [Muungano wa Vituo vya Afya ya Jamii vya Pennsylvania \(PACHC\)](#) upate Kituo cha Afya Kilichoidhinishwa na Serikali ya Kitaifa.

